

# Mamba anazama

ABI  
oni'  
sia.  
Kwenye maji ya bahari, yamepwaa hadi kingo,  
Kwa hicho chake kiburi, awaza angiyepango!  
Yuamutaka Kahari, kimekatika kipingo,  
Mamba na chake kiburi, anazama aangamiya.

Kwa kudhuluma kwa migambo, akicheuwa hasama,  
Akijita nguli Rambo, anakaribia koma,  
Karibu liwa kitambo, kwa tanuri anahema,  
Mamba na chake kiburi, azama aangamiya.

Anabaki kulalama, miswada anaibiwa,  
Alijiona ulama, wengine hakuwajuwa,  
Wamwemesha kinguruma, hatambuwi pa kutuwa,  
Mamba na chake kiburi, azama aangamiya.

Aliwadharau umma, leo hino ajutiya,  
Ataka apawe nema, hali ghuri katwachiya,  
Fakhiri wanamtema, mbali wamukataliya,  
Mamba na chake kiburi, azama aangamiya.

RAMADHAN SAVONGE  
'Malenga wa Nchi Kavu'  
Chuo Kikuu SEKU, Kitui